# Kurejeshwa




MKUSANYIKO WA SALA, ILIYOANDIKWA NA WASICHANA WA JESHI LA WOKOVU KWA ULIMWENGU



# Unaamini wasichana?

## JE, MNAAMINI KWAMBA WASICHANA WANAO UWEZO WA KUIFANYA DUNIA KUWA MAHALI PAZURI ZAIDI? TUNAAMINI!

Kila mwaka, Umoja wa Mataaifa hutambua nguvu, uthabiti na ushawishi chanya wa wasichana duniani kupitia kwa Siku ya Kimataifa ya Msichana. Siku hii vile vile huongeza ufahamu wa vikwazo wanavyo kabiliana navyo wasichana na huimarisha mafanikio yao. Mwaka huu, Tume ya Kimataifa ya Haki za Jamii inaitumia siku hii kuzingatia athari chanya zinazoweza kuletwa na wasichana kwenye uumbaji wa Mungu kupitia kiini cha "Rejesha: Wasichana wanayajali Mazingira".

## TUNATAKA MAISHA BORA YA BAADAYE KWA AJILI YA WASICHANA WETU NA KWA AJILI YA DUNIA YETU.

Tunaishi kati ya mgogoro wa hali ya hewa. Mwenedo wa sasa wa dhoruba mbaya, ukame wa kupitiliza, kupanda kwa kimo cha maji baharini na mfumo wa ikolojia uliogawanyika una athari mbaya kwa usalama, maisha, afya maji safi na mengi mengi. Majanga haya humuathiri kila mmoja, lakini wanawake na wasichana ni baadhi ya wanao athirika zaidi. Mara nyingi wasichana ndiyo wa mwisho kula au kuokolewa katika janga.Hukabiliana na hatari kubwa zaidi kwa afya zao na usalama wao kwani mfumo wa usafi wa mazingira huathirika nao hubeba mzigo mzito unaoongezeka wa kazi za nyumbani wakati rasilimali zinapungua.

Kupitia kwa uzoefu huu, wasichana wanatoa ufahamu wa thamani na masuluhisho katika kutengeneza mfumo rafiki kwa kuishi wa ikolojia, kusimamia vizuri hali ya hewa na athari zake, na kuponya sayari yetu. Ingawa mara nyingi wao hawaonekani kama waanzilishi, wajasiriamali na wafanya maamuzi, wasichana ni msingi katika kujenga siku zetu endelevu za baadaye.

Unavyofuata maombi haya, fikiria kuhusu sababu za haki ya jamii unazoziinua mbele za Mungu:  kupata usawa wa jinsia na kuwawezesha akina mama na wasichana, kuchukua hatua muhimu ili kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa na kuyajali maisha yaliyo chini ya maji na maisha juu ya ardhi.





# Mbingu ni mali yako, nchi nayo ni mali yako, ;

"MBINGU NI MALI YAKO, NCHI NAYO NI MALI YAKO, ULIMWENGU NA VYOTE VIUJAZAVYO, NDIWE ULIYEUPIGA MSINGI WAKE" (ZABURI 89:11).
.

Kama wafuasi wa Kristo, tunaamini Mungu ni Baba yetu na Muumba wetu. Yeye anawajali watu wake wote, kama anavyovijali viumbe hai vyote, nasi tumepewa dhamana ya kuijali dunia na kila kilichomo ndani yake. Imewekwa wazi na madhara tuyaonayo katika dunia yetu, sio kila mara tumeheshimu mwito huo katika maisha yetu na hivyo tunalazimika kufanya kazi ili kurejesha uhusiano wetu na uumbaji wa Mungu ili udhihirishe utunzaji wenye upendo na wenye kujali.

Kabla hatujaanza safari hii ya maombi duniani kote, tendo linalokuza sauti za wasichana kutoka mabara mbalimbali, desturi na yaliyomo, hebu tuchukue muda kidogo kukumbuka kwamba sisi sote tunayo sehemu ya kufanya, bila kujali sisi ni nani. Tunapofanya ili kurejesha uumbaji wa Mungu na kujenga ufalme wake hapa duniani, hebu tusisahau kwamba sisi sote tumo ndani ya hili pamoja.



# Tunaanza safari yetu ya maombi huko Ulaya,

NA ASKARI KIJANA WA KOMANDI YA UHISPANIA NA URENO. BINTI WA MIAKA KUMI NA MITATU ANA ANAISHI GRAN CANARIA, VISIWA VYA CANARY, VINAVYOJULIKA KWA AJILI YA HALI YA HEWA YA KITROPIKI KIASI, ARDHI YA MIAMBA NA MANDHARI NZURI ZA BAHARI. **ANA ANAANZISHA MUDA WETU WA MAOMBI:**

Mpendwa Yesu,




Nashukuru kwa nafasi ya upendeleo uliyotupa sisi ili tuutunze uumbaji wako, lakini naona kwamba sio kila mara tumeifanya vema kazi uliyotupa.

Tunaomba utusamehe kwasababu uumbaji unateseka kwasababu yetu sisi na mitindo ya maisha yetu.

Tusaidie tuweze kuyatunza mazingira na tuwe na mioyo ya huruma kwa wanyama.

Mungu, asante kwa tumaini unalotupa katika Neno lako kwamba siku moja uumbaji utakombolewa.

Katika jina la Yesu,
Amina.

# Maombi haya yametolewa na msichana wa miaka kumi na minne Susan...

SUSAN ANAISHI UGANDA, AFRIKA, NA ANAJUA KITU FULANI KUHUSU MANDHARI YA KIPEKEE YA ARDHI INAYOONYESHA MILIMA, MISITU, MAPOROMOKO YA MAJI, MAZIWA NA MILIMA. **TUNAUNGANA NA SUSAN KATIKA MAOMBI:**

Baba mwema na wa mbinguni,

Nakuja kwenye uwepo wako kukushukuru kwa ajili ya dunia yetu na kila kilichomo ndani yake. Naomba utuumbie ndani yetu akili ya kujali uumbaji wako. Naomba kwa ajili ya viwanda vinavyohimizwa na watumiaji, kwamba watakuwa waangalifu kuhusu mazingira, na watafanya kazi ili kuviweka viumbe hai vyote viwe salama kutokana na hatari zinazotokana na madhara ya mazingira na ongezeko la joto duniani.

Nakuomba , muumba wa ulimwengu, ili tuwe na mioyo inayokumbuka inayotambua jinsi ukataji miti ovyo unavyoathiri vibaya mfumo asilia wa ikolojia. Naomba kwamba viongozi wa serikali duniani watahusika kivitendo kuponya mazingira kwa kupanda miti ili kusaidia kurejesha misitu na kutambua hitaji muhimu la mazoezi ya kilimo bora.



Naomba uwaatamie kiungu viongozi wote wa madhehebu uwafanye wawe jasiri kuunga mkono uhifadhi wa hali ya asili. Pamoja hebu tuongeze ufahamu na tutengeneze mipango ya msaada na yenye kugusa watu, inayofundisha watu jinsi gani kuyatunza mazingira yao.

Naomba utupe sisi wasichana nguvu na hekima ili tutunze na tuirejeshe sayari yetu, tukileta mabadiliko katika dunia yetu.

Katika jina la Yesu naomba,
Amina.

# Huko California Kaskazini, Marekani...

AKINA DADA, LIA NA ALANA, WANATUSHIRIKISHA MAOMBI KUTOKA NYUMBANI KWAO HUKO CALIFORNIA KASKAZINI. WASICHANA HAWA WANATAFAKARI MATOKEO YA MOTO WA MISITU YA KARIBU AMBAO UMEKUWA UKIWAKA MIEZI YA HIVI KARIBUNI, IKIDHURU NA KUHARIBU MIJI, MAJENGO, MAISHA NA WANYAMAPORI. INGAWA ANGA KWA SASA IMEJAA MOSHI, **MADADA HAWA WANATAMBUA KWAMBAMUNGU BADO ANATAWALA:**

Mpendwa Baba wa Mbinguni,

Asante kwa uhai – uhai tunaouona ndani ya kila mmoja, uhai tunaouona kutuzunguka juu ya ardhi, ndani ya bahari na angani. Asante kwa uumbaji wako maridadi.



Tusaidie tutekeleze sehemu yetu katika kuhifadhi na kutunza mazingira tunamoishi; kulinda na kuwa werevu katika kutumia rasilimali tulizo nazo.

Tusaidie tusiyachukue haya kwa wepesi, kwani kufumba na kufumbua, vitu hivi vinaweza kutoweka.

Tunaomba leo ulete utulivu kwa pepo zinazosambaza moto katika eneo letu. Sisi sote tunaathirika kwa namna moja au nyingine, kwa hiyo tunaomba mkono wako wenye nguvu utufunike na kutulinda sisi sote. Tunakuamini na tunajua kwamba wewe unatawala.

Katika jina la Yesu,
Amina.

# Maombi yafuatayo yanatokea Asia Kusini...

MSICHANA WA MIAKA KUMI NA MINNE MINNAL CHRISTIANA, WA TERITORI YA INDIA KATI, ANASIMAMA KATIKA SHAMBA LA KUPENDEZA LENYE MIFUGO KATIKA MALISHO KWA FURAHA KULE NYUMA. **MINNAL ANATOA MAOMBI YAKE:**

Mungu wa Uumbaji,

Tunakushukuru na tunakutukuza kwa kutupa dunia hii nzuri! Tuepushe na kutojali ili baraka zako za hewa safi, maji safi na ardhi tajiri ziwe urithi wa kila kitu kilicho na pumzi ya uhai. Tunaomba kwamba kizazi kimoja kitatangaza hadi kizazi kingine maajabu ya kazi zako katika Yesu Kristo.

Dunia ni yako, na umeamrisha pepo na bahari. Tusaidie tuachane na matumizi ya mahitaji ya plastiki na twende kwenye tabia ambazo ni rafiki kwa mazingira. Tusaidie tufuate uongozi wako katika kuitunza dunia unayoipenda.



Asante kwa maji yaliyopo duniani, kwa mvua inayohifadhi maisha, maziwa na bahari za kina, tusaidie kukumbuka jinsi haya yalivyo na thamani. Tusaidie tufanye kazi pamoja kwa ajili ya maji safi, na tushirikishane vitu hivi na wale wenye kuvihitaji hivi leo. Umeijaza dunia na bahari na anga kwa uhai. Tusamehe kwa kupuuza uumbaji wako, tunajua uharibifu umefanywa kwa kutoyajali makazi na tofauti zetu katika vizazi.

Tusaidie turekebishe maisha na mitindo ya maisha yetu, tu paze sauti zetu ili tupate hatima ya kudumu. Tunataka kuishi vema na kiungwana hapa duniani kwa utukufu wa mwanao.

Katika jina la Yesu nawashirikisha ombi hili,
Amina.

# Katika kisiwa cha mindanao huko Ufilipino...

MAOMBI YETU YA MWISHO YANATOLEWA NA BINTI WA MIAKA KUMI NA MITATU WINCHELL, ANAYEISHI KISIWA CHA MINDANAO HUKO UFILIPINO. KISIWA KIMEZUNGUKWA NA BAHARI NNE, NA MILIMA, NYANDA, MAZIWA NA MAPOROMOKO YA MAJI NI YA KAWAIDA KWA MAZINGIRA YANAYOWAZUNGUKA.

**Muumba wetu na Baba mwenye nguvu,** na kushukuru kwa dunia maridadi na ya ajabu uliyotuumbia na utajiri wote uliomo. Miti mizuri hutupa hewa safi, lakini siku hizi dunia uliyoiumba inakabiliwa na shida kubwa ya kukosa mpango inayosababishwa na roho zetu zisizojali na utashi wa watu binafsi. Hatuwezi kukataa kwamba wengi wana mateso yaliyosababishwa na roho zetu sumbufu.

Watu hawafikirii na hawajali matumizi yao ya plastiki. Mito mingi hivi sasa imechafuliwa. Hapa na sasa hivi nchi inakumbwa na mafuriko kwasababu ya ukataji miti usio halali. Kama msichana mdogo, kwa unyenyekevu nakujia nikiomba msamaha. Tusafishe na udhalimu wetu wote na roho ya ubinafsi.



Naomba kwa ajili ya uongozi na hekima yako iwe juu ya wasichana wote wadogo duniani kote tutoke kwenye maeneo ya starehe zetu na tuwe makini kuona matatizo yanayokabiliwa na uumbaji wako. Tupe hekima tufanye uchaguzi ulio bora, tukusudie kuyatunza mazingira yetu. Tupe roho ya kujiachilia, kuheshimu, kutunza na kuthamini dunia hii maridadi.

Tufanye tuwe mawakili wema wa uumbaji wako, Baba. Tuongezee hamu ya kuifanya dunia iwe mahali pazuri zaidi pa kuishi na mahali kizazi kijacho kitafurahia.

Yote haya naomba katika jina lako, Yesu,
Amina.

# Asante

**HUDUMA YA AKINA MAMA YA KIMATAIFA** INASHUKURU WASICHANA AMBAO WAMEPAZA SAUTI ZAO KWA KUSUDI HILI. TUNAMSIFU MUNGU KWA AJILI YA **ANA, SUSAN, MINNAL, LIA, ALANA NA WINCHELL** NA TUNAMSHUKURU MUNGU KWA VIONGOZI WAO KUWATIA MOYO NA KUWEKEZA. TUNAOMBA KWA AJILI YA MAENDELEO YAO ENDELEVU NA KUENDELEA KWA HUDUMA YAO KAMA WAUMINI WADOGO WA JESHI LA WOKOVU.

**TUME YA HAKI ZA KIJAMII YA JESHI LA WOKOVU**
HTTPS://WWW.SALVATIONARMY.ORG/ISJC

**HUDUMA YA AKINA MAMA YA KIMATAIFA**
FACEBOOK: SALV ARMY WOMEN
INSTAGRAM: SALVARMYWOMEN